


# Wakali wao!

HIZI NDIZO FAIDA ZA WANYAMA PORI

fikrapevu @fikrapevu @fikrapevu

# BUSATI

Ukweli na Uhakika

Tovuti www.busati.mali.co.tz/ISSN 3456-3421 Na. 38, Jumanne Machi 4, 2025 Bei Tsh. 1000/= Ksh 100

## UZALISAJI MAKAA YA MAWE...

# Rais Samia aipaisha Ruvuma kwa mapato

- HII NI KATIKA KIPINDI CHAKE CHA MIAKA MINNE YA UWEPO MADARAKANI
- AIFANYA RUVUMA IWE JUU KIMAPATO KUPITIA MAKAA YA MAWE
- MADINI HAYO YAMEUZWA NDANI YA AFRIKA, ULAYA NA ASIA



"Kwa data zilizopo zinaonyesha kuwa, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali iliuza tani 1,356,249.84 za makaa ya mawe zenye thamani ya zaidi ya Dola milioni 144.9 za Marekani.

# Cheka tu simu yako inakuvuruga

Sio jambo la ajabu kujua kwamba kwa sasa kuna watu hasa vijana ambao matumizi



ya simu yameathiri sana uwezo wao hata kuweza kutangamana kwa njia ya kawaida.

Wamezoea kutumia simu na wakati wasipokuwa na simu zao...UK.10

## Kibong'oto Taasisi Magonjwa Ambukizi

NA MWANDISHI WETU

**WAZIRI wa Afya Jenista Mhagama amesema Hospitali Maalum ya Tiba ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto inatarajiwa kuwa Taasisi ya Magonjwa Ambukizi ambayo itakwenda sambamba na uimarishaji wa mifumo ya huduma za tiba ya magonjwa hayo.**

Waziri Mhagama amesema hayo juzi, alipofanya ziara katika Hospitali ya Kibong'oto kwa lengo la kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ambayo Serikali imetoa fedha ikiwa ni pamoja na eneo la uzalishaji wa gesi tiba na ununuzi wa mashine za kisasa za kuchomea taka.

"Tumejipanga kwenye Sekta ya Afya, pamoja na huduma nyingine za afya za kibobezi, tunataka kuuthibitishia ulimwengu kwamba hata kwenye eneo hili la magonjwa ambukizi kama nchi tumejizatiti vizuri kwa kuhakikisha mifumo yetu ya tiba iko imara," amesema Waziri Mhagama.

Amesema, magonjwa hayo ambukizi yanaweza kuibuka mahala popote katika nchi, hivyo kwa uwekezaji mkubwa uliofanywa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan unaiwezesha Tanzania kupambana na magonjwa hayo kwa kuzingatia utaratibu na mifumo ya afya iliyopo.

"Kwa hiyo hapa sasa kitakuwa ni kituo cha umahiri katika eneo hilo la magonjwa ambukizi, ninafurahi nilipokuja kuzindua Bodi tulikubalia ni lazima tuwe na mpango mkakati unaotekelezeka, ambao utatufikisha kwenye malengo endelevu na sasa naona utekelezaji wake umeanza," amesema Waziri Mhagama.

Aidha Waziri Mhagama amesema Serikali imewekeza zaidi zaidi ya Shilingi Milioni 550 kwa ajili ya kujenga sehemu maalum ya kuchomea taka pamoja na ununuzi wa mashine maalum ya kisasa ambao una uwezo wa kuteketeza taka zaidi ya Kg 400 kwa saa moja katika eneo hilo.

Pia, Waziri Mhagama amesema Serikali kupitia Wizara ya Afya imewekeza zaidi ya Bilioni 1.6 kwa ajili ya kutengeneza mradi wa kuzalisha gesi tiba ambao mradi huo umeshakamilika na kuanza kufanya kazi katika Hosoitali hiyo, ambao umesaidia kuokoa fedha za kuagiza gesi hiyo kutoka nje.

# Gwajima atoa la moyoni

NA MWANDISHI WETU

**WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Dkt. Dorothy Gwajima, amewataka waandishi wa habari kuongeza kasi ya kuandika habari za malezi, makuzi na Maendeleo ya Awali ya Watoto ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto ya 2021/22-2025/26.**

Dkt. Gwajima amesema hayo hivi karibunijijini Dodoma wakati akizungumza waandishi wa habari Vinara wa Malezi na Makuzi ya Awali ya Watoto, Wamiliki wa Redio za Kijamii na Waratibu wa Klabu za Waandishi wa Habari kutoka Mikoa 26 ya Tanzania Bara.

Amesema waandishi wa habari wana wajibu wa kipekee kupitia kalamu taaluma zao, vyombo vya habari katika kuhamasisha jamii, kuchagiza uwajibikaji wa wadau wa watoto na kuhakikisha kuwa changamoto zilizopo zinajadiliwa na kupatiwa ufumbuzi.

"Tafiti zinaonesha kuwa redio ndio chombo cha habari kinachosikilizwa na idadi kubwa ya wanajamii. Hivyo, wamiliki wa redio na waandaji wa vipindi vya kueliemisha jamii.

"Tumieni fursa hii ya mafunzo kuhakikisha kuwa mnaandaa vipindi vyenye ubora, pamoja na ushirikishwaji thabiti wa wadau na Serikali, ili maudhui ya vipindi yasaidie jamii kufanya maamuzi sahihi kuhusu malezi ya watoto."

Dkt. Gwajima ameongeza kwamba wanahabari wanatakiwa kuandika habari zinazohusu uanzishaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana kwenye jamii vikiwemo vile vinavyoanzishwa na kumilikiwa na jamii yenyewe kwa lengo la kutoa fursa kwa watoto kupata mwanzo mzuri wa malezi na kuwapa nafasi wazazi au walezi.

## NIDA yapewa maelekezo ya kutosha

NA MWANDISHI WETU

**WAZIRI wa Mambo ya Ndani, Innocent Bashungwa ameitaka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kushirikiana na Idara ya Uhamiaji pamoja na Idara ya Wakimbizi kushughulikia maombi ya Vitambulisho vya Taifa kwa wananchi wa mikoa ya pembezoni ambapo ametaka waliokidhi vigezo wazalishiwe vitambulisho na watakaothibitika hawana vigezo wapewe taarifa.**

Bashungwa ametoa maagizo hayo hivi karibuni jijini Dodoma wakati alipokutana na Menejimenti ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kujadili utendaji kazi na uboreshaji wa utoaji huduma wa Mamlaka hiyo.

"Muendelee kushirikiana na Idara ya Wakimbizi na Uhamiaji, kwa mikoa kama Kigoma na Kagera kushughulikia maombi yenye changamoto bila kuvunja sheria, yule ambae hajakidhi mwambieni lakini yule mwenye vigezo vya kupata kitambulisho basi apewe," amesisitiza Bashungwa.

Aidha, Bashungwa amemtaka Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kuongeza ubunifu wa kuhakikisha vitambulisho vya Taifa vilivyozalishwa vinawafikia Wananchi husika pamoja na kuongeza kasi ya Usajili na utambuzi wa wananchi waliosalia kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi 2022.

Kwa Upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa NIDA, James Kaji ameeleza kuwa NIDA inaendelea na zoezi la kusambaza vitambulisho ambavyo vilikuwa havijawafikia Wananchi ambapo kufikia tarehe 10 Februari 2025 jumla ya vitambulisho 1,507,796 vimesomeshwa kwenye mfumo na wamiliki wa vitambulisho 918,216 wameshatumiwa ujumbe mfupi ili kuchukua vitambulisho vyao.



# Dk. Samia aipaisha Ruvuma kwa mapato

NA ALBANO MIDELO, Songea

**HUYU ndiye Rais Dkt. Samia! Hili ni neno unaloweza kulitumia kutokana na kuiwezesha Ruvuma kupanda juu kimapato, huku chanzo kikuu kikiwa ni uzalishaji wa madini ya makaa ya mawe, unaoendelea kwa kasi mkoani humo.**

Hii yote ni katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wake, ambapo tani kadhaa zimeuzwa na kuiingizia Serikali mapato makubwa, hivyo kufanya mkoa huo kufanikiwa kuchangia pa kubwa katika Pato la Taifa.

Kwani, katika kipindi hiki cha miaka minne cha uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, uzalishajili wa madini ya makaa ya mawe ndani ya Mkoa wa Ruvuma umeendelea kuwa chanzo muhimu cha mapato ya serikali.

Kwa data zilizopo zinaonyesha kuwa, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali iliuza tani 1,356,249.84 za makaa ya mawe zenye thamani ya zaidi ya Dola milioni 144.9 za Marekani.

Afisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Ruvuma, Mhandisi Alphonce Bikulamchi, amesema kupitia mauzo hayo, serikali ilikusanya mrabaha wa Dola 3,937,434.98 na ada ya ukaguzi ya Dola 914,034.68.

Madini hayo yameuzwa ndani ya nchi na kusafirishwa katika nchi jirani, barani Ulaya na Asia kupitia bandari za Mtwara na Dar es Salaam.

"Ofisi ya Afisa Madini Mkazi wa Ruvuma imeendelea kutoa leseni za uchimbaji na biashara ya madini, ikiwemo leseni za uchimbaji mdogo (PML) na leseni za madini ya biashara kwa madalali (Dealers na Brokers).

"Idadi ya leseni zilizotolewa imekuwa ikiongezeka, ambapo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 2024/2025, mkoa una jumla ya leseni 144 za utafutaji madini na uchimbaji mkubwa na wa kati," alisema Mhandisi Bikulamchi,

Kwa mujibu wa Bikulamchi,Katika ukusanyaji wa maduhuli, Ofisi ya Madini Mkoa wa Ruvuma ilikusanya jumla ya shilingi 105,120,541,415.03 kati ya mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 2024/2025, sawa na asilimia 126 ya lengo la makusanyo.

## Baraza la Ushauri Kazi lazinduliwa

NA MWANDISHI WETU

**WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu- Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Ridhiwani Kikwete amezindua Baraza la Ushauri wa masuala ya Kazi, Uchumi na Jamii (LESCO) jana jijini Dodoma.**

Akizungumza wakati wa Uzinduzi wa Baraza hilo, Kikwete amewataka wajumbe wa baraza hilo kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia weledi na uzoefu katika masuala ya Kazi, Ajira, Uchumi na Jamii huku wakitanguliza mbele maslahi ya nchi, uzalendo, uadilifu, haki na wajibu wa pande zote ili kukidhi falsafa ya serikali ya awamu ya sita ya katika kuhudumia wananchi.

"Ni matarajio yangu baraza litatekeleza majukumu yake kwa ufanisi ili kufanikisha azma ya serikali inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kujenga Uchumi, kukuza ajira na kuhudumia jamii," amesema.

Vile vile, amesisitiza baraza hilo kutoa maoni na ushauri kuhusu sera, sheria, mikakati, kanuni na miongozo itakayosaidia kukuza kazi za staha, kuendeleza na kujenga Uchumi, kuongeza tija na uzalishaji kwa ujumla.

Aidha, kwa mujibu wa Sheria za Kazi Kifungu (5) Sura 300, LESCO ina majukumu mengi inayoyatekeleza ikiwa ni Pamoja na kumshauri Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Kazi na Ajira kuhusu masuala yote yanayohusu Kazi, Ajira, Uchumi na Jamii.

## Waziri Harusi ashauri taasisi Z'bar

NA MWANDISHI WETU

**WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Harusi Said Suleiman, amezitaka taasisi zenye uwezo kutafuta miradi ya kuwawezesha makundi maalum ili yawajibike kiuchumi na kuepukana na utegemezi.**

Waziri Suleiman alitoa wito huo wakati wa hafla ya kukabidhi futari kwa familia 800 za watu wenye ulemavu, hafla iliyoandaliwa na Taasisi ya Nour Al-Yaqin Foundation katika Ukumbi wa Dk. Ali Mohammed Shein, Tunguu, Zanzibar.

Alisema uzoefu unaonesha kuwa watu wenye ulemavu, wajane, mayatima na wasiojiweza mara nyingi hupewa misaada ya mahitaji ya msingi ambayo hutumika na kuisha, hivyo kubaki wakisubiri msaada mwingine.

"Umefika wakati wa taasisi kuangalia miradi mbadala inayoweza kuwasaidia kujiendesha kimaisha na kukidhi mahitaji ya familia zao. Wapo wenye ulemavu wanaoweza kufanya kazi na kujipatia kipato endapo watawezeshwa," alisema Waziri Suleiman.

# Mazingira ya asili yanapogawanyika

**MPENDWA msomaji wa makala hizi za wanyamapori karibu katika makala hii inayohusu kugawanyika kwa mazingira ya asili yaan Habitat Fragmentation. Neno mazingira ya asili maana yake ni ardhi ambayo inahifadhi aina mbalimbali za mimea, wanyama, wadudu na vinginevyo.**

Kabla ya kuharibiwa au kubadilishwa matumizi yake kugawanyika kwa mazingira ya asili ni kitendo cha eneo kubwa la mazingira ya asili kubadilishwa na kuwa vipande vidogovidogo vilivyojitenga. Vipande hivi huwa kila kimoja na mandhari tofauti ukilinganisha na lile la asili.

Kugawanyika kwa mazingira ya asili hujumuisha upotevu wa mazingira pamoja na mabadiliko katika muundo wa mazingira. Mchakato huu husababisha sehemu ambazo hutenganisha kipande kimoja na kingine kuongezaka kwa viwango vya mwanga, joto, kasi ya upepo na pia hali ya unyevu

Kugawanyika kwa mazingira ya asili imekuwa ni tishio kubwa hapa duniani linalopelekea upotevu wa viumbehai. Wanyamapori wengi wana mazingira yao ya asili ambayo hutumia kufanyia shughuli zao za kila siku lakini kutokana na kugawanyika kwa mazingira ya asili hupelekea kupungua kwa ukubwa na ubora wa makazi na maeneo ya chakula na pia maeneo ya kuzaliana.

Hifadhi nyingi nchini zinakabiliwa na tatizo la kugawanyika kwa mazingira ya asili kwa sababu ya shughuli za binadamu ndani na karibu na hifadhi. Hivyo mchakato huu huleta athari nyingi katika shughuli za kiuhifadhi.

Mchakato huu unaathiri zaidi spishi ambazo hutegeemea maeneo makubwa kwa ajili ya kustawi kama Wanyama wakubwa kama tembo na ndege na wanyama kama nyumbu wanaohama kwa misimu hivyo hukabiliwa na changamoto ya kupungua kwa uwezo wa kufikia rasilimali.

Ujenzi wa Barabara, reli, na miundombinu mbalimbali katika maeneo ya hifadhi au karibu na hifadhi huweza kusababisha kugawanyika kwa mazingira ya asili kwa kuvunja maeneo ya asili na kuzuia au kuathiri shughuli za wanyamapori.

Mabadiliko ya tabia ya nchi yanaweza kusababisha kugawanyika kwa eneo la asili , kwa mfano ongezeko la joto au ukame katika misitu linaweza kusababisha kupunguza eneo la msitu kwani baadhi ya miti hufa na kuacha uwazi kati ya sehemu moja na nyingine hivyo msitu unakuwa umegawanyika.

Mito husababisha kugawanyika kwa mazingira ya asili katika hifadhi kwa kuwa kama kizuizi cha kijiografia ambapo hugawanya ardhi na kuwa kama mipaka kati ya sehemu moja na nyingine hivyo kuzuia shughuli mbalimbali za wanyamapori.

Chanzo: www.britanica. ikionesha mto umegawanya eneo la msitu na kuwa ni vipande viwili tofauti.

Kugawanyika kwa mazingira ya asili kunaweza sababisha upungufu wa maeneo ya makazi ya wanyamapori. Hali hii hutokea pale ambapo eneo la wanyamapori la asili liliweza kuwamudu wote kupata makazi na mahitaji yao muhimu kama chakula, maji na maeneo ya kuzaliana lakini kutokana na kugawanyika kwa eneo.





# Ukitaka kufanikiwa katika biashara

**KUFANIKIWA katika biashara kunahitaji zaidi ya wazo zuri; kunahitaji nidhamu, maarifa, na ufuataji wa kanuni muhimu zinazosaidia kukuza na kuendesha biashara kwa ufanisi.**

Hapa kuna kanuni za msingi ambazo zinaweza kukusaidia kufanikisha biashara yako.

Mpango wa Biashara

Mpango wa biashara ni ramani ya mafanikio yako. Unapanga malengo yako, mikakati, na njia za kufanikisha malengo hayo. Hakikisha mpango wako ni wa kina, unajumuisha masuala ya kifedha, utafiti wa soko, na njia za kutatua changamoto.

**Soko Lako**

Maarifa kuhusu wateja wako ni msingi wa mafanikio. Tafuta kujua mahitaji, matakwa, na changamoto za wateja. Uelewa huu utakusaidia kutoa bidhaa au huduma zinazokidhi matarajio ya wateja wako.

**Busara**

Udhibiti mzuri wa rasilimali zako, iwe ni fedha, muda, au wafanyakazi, ni muhimu kwa mafanikio ya biashara. Epuka matumizi yasiyo ya lazima na wekeza kwenye maeneo yenye faida kubwa.

**Jifunze**

Ulimwengu wa biashara hubadilika kila siku. Jifunze mbinu mpya, fuatilia mwelekeo wa soko, na tafuta maarifa mapya kupitia semina, vitabu, au wataalamu wa biashara. Maarifa mapya huongeza uwezo wako wa kushindana sokoni.

**Utafiti**

Elewa nguvu na udhaifu wa washindani wako. Utafiti huu utakusaidia kuboresha bidhaa au huduma zako na kutoa thamani ya kipekee kwa wateja wako.

**Huduma Bora**

Wateja ni moyo wa biashara yako. Hakikisha wanapata huduma bora, na tatua malalamiko yao kwa haraka. Wateja wenye furaha si tu watarudi, bali pia watakutangaza kwa wengine.

**Kuwa Mbunifu**

Ubunifu ni silaha muhimu katika biashara. Tafuta njia mpya za kufanya kazi, tengeneza bidhaa mpya, au boresha huduma zako ili kuendana na mahitaji yanayobadilika ya wateja.

**Dhibiti Fedha**

Fedha ni uti wa mgongo wa biashara. Hakikisha unadhibiti mapato na matumizi yako kwa usahihi. Tumia programu za uhasibu au mshauri wa fedha ili kuhakikisha usimamizi mzuri wa fedha zako.

**Mtazamo**

Mafanikio katika biashara hayaji mara moja. Wekeza muda na juhudi katika kujenga msingi thabiti wa biashara yako. Epuka kutafuta faida ya haraka bila kufikiria athari za muda mrefu.

**Nidhamu na Mshikamano**

Mafanikio ya biashara yanahitaji nidhamu kali. Fuata ratiba zako, maliza kazi zako kwa wakati, na hakikisha unadumisha maadili bora. Shikamana na malengo yako hata unapokutana na changamoto.

**Hitimisho**

Biashara yenye mafanikio inahitaji maandalizi mazuri, kazi ngumu, na uwezo wa kuhimili changamoto. Kwa kufuata kanuni hizi, unaweza kujenga biashara thabiti inayokua na kuleta faida.

Kumbuka, safari ya mafanikio inaanza na hatua ndogo, lakini inahitaji msukumo wa kila siku kufanikisha malengo yako.



# Miti lazima uilinde ili ikuheshimu

**MITI ni rasilimali muhimu kwa ustawi wa maisha ya viumbe hai na mazingira. Kutokana na uwezo wao wa kutoa hewa safi, kuboresha afya ya udongo na kutoa makazi kwa wanyama, miti ni sehemu muhimu sana ya mfumo wa ikolojia.**



Aidha miti ina nafasi kubwa katika maendeleo ya uchumi na afya ya kijamii.

**1. Faida za Miti kwa Mazingira**

Miti inachukua kaboni dioksidi ($CO_2$) kutoka kwenye hewa na kutoa oksijeni ($O_2$), ambayo ni muhimu kwa uhai wa viumbe hai.

Pia miti husaidia kunyonya uchafuzi wa hewa na chembechembe zinazoathiri afya zetu na hivyo kuchangia katika kupunguza magonjwa yanayosababishwa na hewa chafu.

Miti husaidia kupunguza joto kwa kutoa kivuli na kubadilisha mzunguko wa hewa karibu nao. Katika maeneo ya mijini, miti hupunguza athari za joto linalosababishwa na majengo na barabara kwa kupunguza joto la hewa.

Pia miti hucheza nafasi muhimu katika kudhibiti mabadiliko ya hali ya hewa kwa kunyonya gesi za joto. Mizizi ya miti husaidia kuimarisha udongo na kuzuia mmomonyoko unaosababishwa na mvua na upepo.

Hii ni muhimu sana kwenye maeneo ya milima na mabonde ambapo mmomonyoko wa udongo unaweza kusababisha maporomoko ya ardhi na mafuriko.

Miti husaidia katika mzunguko wa maji kwa kunyonya maji kutoka kwenye ardhi na kuyaachia kwenye anga kwa njia ya uvukizaji.

Hii husaidia katika kuongeza unyevu hewani, na kuchangia katika mvua ambayo ni muhimu kwa kilimo na viumbe vingine.

**2. Umuhimu wa Miti**

Miti mingi ni chanzo cha dawa za asili zinazotumika kutibu magonjwa mbalimbali. Miti kama mwarobaini, mkaratusi, na mchaichai ni maarufu kwa uwezo wao wa kutibu maradhi.

Matumizi ya miti katika tiba asili ni njia bora ya kupata matibabu yasiyo na madhara makubwa kwa mwili.

Uwepo wa miti husaidia kuboresha afya ya akili. Uchunguzi umeonyesha kuwa kutembea au kuwa karibu na maeneo yenye miti husaidia kupunguza msongo wa mawazo na kuboresha hali ya mtu kisaikolojia.

Hii ni kwa sababu miti na uoto wa asili huleta utulivu na hali ya amani.

Miti huondoa uchafuzi wa hewa unaoweza kusababisha matatizo ya kupumua kama vile pumu na mzio. Miti yenye majani mengi husaidia kusafisha hewa kwa kunyonya vumbi na kemikali hatari ambazo huathiri afya ya binadamu.

3. Faida za Miti

Miti ni chanzo cha ajira kwa jamii nyingi kupitia sekta za kilimo, ufugaji wa miti (misitu), na uuzaji wa mbao. Misitu ni chanzo kikuu cha mbao, karatasi, na bidhaa nyingine za misitu ambazo zinauzwa ndani na nje ya nchi, na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi.

Miti ni chanzo cha nishati kupitia kuni na mkaa ambao hutumika kupikia katika sehemu nyingi za vijijini na mijini. Hata hivyo, ni muhimu kutumia nishati hii kwa njia endelevu kwa kupanda miti zaidi ili kuepuka uharibifu wa misitu.

Miti hutoa malighafi muhimu kwa viwanda, kama vile mbao kwa ajili ya ujenzi, karatasi, na bidhaa za plastiki zinazotengenezwa kwa utomvu wa miti.

Misitu inasaidia kuwepo kwa malighafi kwa bei nafuu na inayopatikana kwa urahisi.

**4. Miti na Mfumo wa Ikolojia**

Misitu ni makazi ya aina mbalimbali za wanyama, ndege, na wadudu. Miti hutoa chakula na makazi kwa viumbe hawa, hivyo kuhifadhi usawa wa mfumo wa ikolojia.

Viumbe hawa ni muhimu katika mchakato wa kuchavusha mimea na kudhibiti wadudu waharibifu wa mimea.

Miti husaidia kuhifadhi uoto wa asili na aina mbalimbali za mimea na wanyama. Misitu yenye uoto wa asili huhifadhi viumbe hai wengi, na hivyo kudumisha utofauti wa viumbe hai ambao ni muhimu kwa afya na ustawi wa mazingira kwa ujumla.

Miti husaidia kurudisha virutubisho ardhini kwa njia ya majani, magome, na matawi yanayoyodondoka. Haya yanapooza, yanarudisha madini na virutubisho muhimu kwenye udongo, na kusaidia kuongeza rutuba ya ardhi.

**5. Miti na Jamii**

Miti hutoa maeneo ya kivuli ambayo watu wanaweza kutumia kwa mapumziko na burudani.

Hii ni muhimu hasa katika maeneo ya mijini ambako kuna viwango vya juu vya joto kutokana na majengo na barabara. Pia maeneo yenye miti yanaweza kuwa sehemu nzuri za kukutana na kufanya shughuli za kijamii.

Misitu na miti mikubwa ya asili ni vivutio vya utalii. Watalii huvutiwa na mandhari nzuri, na hivyo huchangia mapato kwa nchi.



# Njia 5 za kuokoa mazingira

**BINADAMU anavunja rekodi zote mbaya kuhusu ongezeko la joto duniani. Mifumo dhaifu ya ekolojia inakabiliwa na shinikizo kubwa. Zaidi ya mimea wanyama na viumbe hai wengine milioni 1, wako hatarini kuangamia. Hewa chafu na uchafuzi wa kemikali vinatishia ardhi, bahari na afya yetu.**

Lakini Siku ya Kimataifa ya Mama Dunia, Aprili 22 ni ukumbusho kwamba kuna mengi tunayoweza kufanya, kama watu binafsi, ili kukabiliana na majanga ya aina tatu duniani ya mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa mazingira na bayoanuai, na uchafuzi na taka.

"Kila hatua, hata iwe kubwa au ndogo, ni muhimu kwa sayari," alisema Bruno Pozzi, Naibu Mkurugenzi wa Kitengo cha Mifumo ya Ekolojia cha Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP).

"Dharura ya tabianchi, uharibifu wa mazingira na uchafuzi mbaya zaidi wa mazingira ni visivyoweza kupuuzwa. Tunaweza kubadili hali ya kudorora kwa Dunia lakini tunahitaji kuja pamoja na kila mmoja wetu kutekeleza wajibu wake."

UNEP imetengeneza zana za nyenzo za kuchukua hatua za kushughulikia mazingira kuhusiana na masuala mbalimbali. Hapa kuna mwongozo kuhusu masuala tano kati yake:

**Uisha mifumo ya ekolojia**

Je, wajua kuwa duniani zaidi ya hekta bilioni 2 za ardhi zimeharibiwa? Au kuwa idadi na muda wa ukame kudumu umeongezeka kwa asilimia 29 tangu mwaka wa 2000. Kupata masuluhisho kwa matatizo haya ulimwenguni ni muhimu.

Siku ya Mazingira Duniani tarehe 5 Juni itaangazia uboreshaji wa ardhi, kuenea kwa majangwa na kustahimili ukame. Mwongozo wa Uboreshaji wa Mifumo ya Ekolojia: Mwongozo wa Vitendo vya Kuponya Sayari unaelezea mbinu za kurejesha aina nane muhimu ya mifumo ikolojia - misitu, mashamba, maeneo yaliofunikwa na nyasi na maenao ya savana, mito na maziwa, bahari na maeneo ya pwani, miji na majiji, maeneo ya mboji na milima. Kwa kuchukua hatua hizi zinazopendekezwa, unaweza kuwa sehemu ya #GenerationRestoration!

**Hamasisha Mabadiliko ya Tabianchi**

Ulimwengu unakabiliwa na dharura ya tabianchi, "ishara ya hatari kwa wanadamu," kwa mjibu wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Uzalishaji wa gesi ya ukaa usipopungua mno, ongezeko la joto linaweza kupita nyuzijoto 2.9 katika karne hii.

Kampeni ya UNEP ya Chukua Hatua Sasa: Hamasisha inaonyesha jinsi wananchi wanavyoweza kulazimisha serikali na mashirika ya biashara kufikia aina ya mabadiliko ya kimfumo yanayohitajika ili kudhibiti ongezeko la joto duniani lisizidi nyuzijoto 1.5 zaidi ya viwango vya kabla ya kuanza kwa viwanda.

**Komesha mlima wa plastiki**

Plastiki imetapakaa kila mahali. Iko katika mavazi yetu, vifaa vya kutumia nyumbani, vifaa vya watoto kuchezea, vifaa vya kufungia chakula, vifaa vya matibabu... orodha hii inaendelea. Ingawa plastiki ina matumizi mengi, mazoea yetu ya kutumia plastiki inayotumika mara moja hudhuru sayari. Inaweza kuchukua maelfu, au maelfu na maelfu, ya miaka kuoza.



Hata hivyo tunaendelea kuzalisha na kutumia tani milioni 430 za plastiki kwa mwaka, theluthi mbili kati yake hujikuta haraka kwa taka zinazotupwa kwenye mazingira, kwa mfano, madampo na kuchafua maziwa, mito, udongo na bahari.

Kwa kufahamu athari za plastiki kwa mabadiliko ya tabianchi, mifumo ya ekolojia, wanyamapori na uchumi, Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa zilikubaliana kuhusu azimio la kuunda a chombo cha kisheria cha kukomesha uchafuzi wa plastiki.

Hii ni pamoja na kupunguza plastiki isiyohitajika, kuchagua kutumia tena badala ya kununua bidhaa mpya, kuunga mkono kampuni zinazounda upya plastiki na kujaribu kupunguza matumizi ya plastiki inayotumika mara moja, na kuziomba serikali kupitisha sera za kuchochea uchumi unaotumia bidhaa tena na tena na kuimarisha mifumo ya kushughulikia taka.

**Kupiga marufuku hewa chafu kutoka angani**

Zaidi ya asilimia 99 ya watu duniani huvuta hewa isiyo salama. Uchafuzi wa hewa ndio hatari kubwa zaidi kwa afya nyakati zetu, na husababisha vifo vya mapema vya takriban watu milioni 7 kila mwaka.

Kukumbana na hewa chafu pia kunaweza sababisha magonjwa ya moyo na mapafu, saratani ya mapafu na kiharusi na magonjwa mengine.

Vichafuzi vya hewa pia hudhuru mazingira yetu asilia, hupunguza usambazaji wa oksijeni katika bahari zetu, na kuifanya kuwa vigumu kwa mimea kukua na kuchangia janga la mabadiliko ya tabianchi.

Siku ya Kimataifa ya Hewa Safi ili kuwa na anga za bluu tarehe 7 Septemba inalenga kuhamasisha kuhusu tatizo hili, huku mwongozo unaoingiliana wa UNEP ukifafanua hatua unazoweza kuchukua ili kupelekea kuwa na hewa safi.

**Panda miti mwafaka, usikosee**

Miti ni ya ajabu." Hufyonza hewa ya ukaa kutoka angani, hulinda na kurutubisha udongo, ni chanzo cha kuni na mbao, na hutoa makazi kwa wanyama, ndege na wadudu wengi.

Si ajabu kuwa upandaji miti, kuboresha mifumo ya ekolojia na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, vimekuwa maarufu sana. Lakini sio rahisi kama inavyosikika.

Kwa mfano, kupanda miti isiokuwa mwafaka mahali pasipofaa kunaweza kudhuru bayoanuai na kusababisha kila aina ya matokeo yasiyokusudiwa. Upandaji Miti na uboreshaji wa mfumo ya ekolojia: kozi ya kina ya UNEP inaweka kanuni tano za msingi za kufanya usikosee.

# TALAKA INAVYOUTIKISA UFALME WA WAZULU

**MAHUSIANO ya kimapenzi ya Mfalme wa jamii ya Wazulu kutoka Afrika Kusini yamezua mjadala nchini humo huku gumzo linalohusiana na maisha yake ya kibinafsi likisambaa kwa kasi kama moto wa nyikani katika jamii hiyo ambayo inakumbatia utamaduni wake.**




Mfalme wa Zulu anasemakana kuvunja kanuni za kitamaduni kwa kutaka kutoa talaka, jambo ambalo haliendani na itikadi za jamii hiyo.

Mume kuwa na wake wengi ni mojawapo ya masuala yanayokubalika katika jamii ya Wazulu, lakini Mfalme Misuzulu kaZwelithini amefanya uamuzi ambao sio wa kawaida kwa kuwasilisha kesi mahakamani ya kutaka kumtalaki mke wake wa kwanza, Malkia Ntokozo kaMayisela.

"Kila mmoja ameshangazwa. Watu hawakutarajia kwamba yangefikia kiwango cha kutaka kutoa talaka,' alisema Profesa Gugu Mazibuko ambaye ni mtaalamu wa utamaduni katika Chuo Kikuu cha Johannesburg huko Afrika Kusini.

'Katika utamaduni wa jamii ya Wazulu, hakuna talaka. Haupaswi kumfukuza mke wako,' alisema.

Mfalme wa Jamii ya Wazulu anayefahamika kama 'Simba wa taifa,' ndiye mwenye kuhifadhi tamaduni za jamii hii ambazo ni za jadi. Tamaduni hizi zimedumisha ndoa na hususan ndoa ya wake wengi kama jambo kubwa kabisa la mafanikio ya ufalme.

Na japo majukumu yake nchini Afrika Kusini ni ya kitamaduni na hayana uzito katika sheria za nchi hiyo, kiongozi huyu wa jamii anasalia kuwa na ushawishi mkubwa katika jamii huku ofisi yake ikipokea ufadhili wa mamilioni ya dola za Kimarekani kutoka kwa serikali kuu.

Mfalme huyo ambaye alikulia katika taifa jirani la Eswatini, alipata masomo yake nchini Marekani na kukabidhiwa wadhifa wa uongozi mnamo 2021. Aidha amekuwa akikabiliwa na utata tangu awali.

Kukabidhiwa kwake mamlaka kulipingwa mahakamani na kaka yake mkubwa ambaye ni wa mama mwingine aliyetaka kupokezwa ufalme huo.

Ndoa yake ya pili, imegonga vichwa vya habari, na jaribio lake kuoa mke wa tatu limegonga mwamba huku kukiwa na ripoti kwamba ana uhusiano kwa kando na mwanamfalem wa kike.

Hata hivyo, kashfa inayozunguka maisha ya kiongozi huyo mwenye umri wa miaka 50 imekuwa ikijadiliwa chini kwa chini hadi pale alipotangaza azma ya kumtalaki mke wake na kuwasilisha ombi rasmi mahakamani mwezi Desemba.

Profesa Madibuko amekiri kwamba kumbukumbu za historia ya Wa Zulu zinaonyesha kwamba kuna mfalme ambaye katika karne ya 20 alimtalaki mmoja wa wake zake, 'ila hilo lilifanyika kimya kimya na kuwa siri kubwa katika familia hiyo ya kifalme,' ikizingatiwa kwamba talaka katika ufamle wa Zulu sio jambo la kawaida.

"Ikiwa uhusiano utavunjika, basi mke huyu ataendelea kuishi katika boma la mfalme. Atapewa eneo lake kando, na hatakuwa na uhusiano an mfalme, ila yeye na watoto wake watatunzwa."

Ilikuwa muda kabla ya kupokezwa ufalme punde tu baada ya kifo cha ghafla cha baba na mama yake miaka minne iliyopita kwamba mwanamfalme (wakati huo) Misuzulu alipomuoa Ntokoto Mayisela.

Wawili hao walikuwa tayari kwenye uhusiano wa kimapenzi na walikuwa tayari ni wazazi wa watoto wawili, ila kwa mujibu wa mtaalamu mwingine wa utamaduni wa jamii ya Zulu, Prof Muza Xulu kutoka chuo kikuu cha Zululand, uamuzi wa kufunga ndoa ulionekana kuharakishwa.

"Ilionekana kwamba mwanafalme hangeweza kuwa mfalme ikiwa hakuw ana mke."

Malkia kaMayisela alitokea familia ya kawaida kama wake wengine wa wafalme wa Kizulu kutoka mji mdogo wa uchimbaji madini katika jimbo la KwaZulu Natal.

"Malkia alimvutia Mfalme katika mgahawa mmoja kwenye mji wa pwani wa Durban alipokuwa akifanya kazi kama muimbaji," alisema Prof Xulu.

Hadhi yake katika familia iliwekwa wazi wakati wa kutawazwa kwa mfalme mnamo Desemba 2022 alipoketi kando yake.

Ila nafasi yake sasa inatishika, anapotaja mume wake kwamba wawili hao hawajaishi pamoja kama mume na mke kwa mwaka mmoja uliopita na kwamba ndoa yao imevunjika.

Kasri ya mfalme ilifuatilizia matamshi yake kwa kutuma mualiko wa ndoa ya Mfamle kwa mke mwingine, Nomzamo Mayeni mwishoni mwa mwezi Januari. Mahari ya bibi harusi inayofahamika kama LOBOLA kwa lugha ya kizulu imeshalipwa – huku ng'mbe wanaothaminiwa sana katika jamii hiyo wakitolewa kama mahari.

Malkia kaMayisela hajapokea haya yote vyema, akitaja kwamba huenda akawasilisha malalamishi ya kutaka ndoa hiyo kutofanyika, hali iliyosababisha ndoa hiyo kuahirishwa.

Ameiambia mahakama kwamba, mfalme ambaye anatambulika miongoni mwa jamii hiyo kama "ingonyama", kumaanisha simba, angekuwa anavunja sheria za ndoa kwa kufunga ndoa ya pili japo mke wa kwanza yupo.

Anasema pia kwamba hatua hiyo inafanyika chini ya ndoa iliyofanyika katika ofisi ya mwanasheria mkuu ambayo haikubaliwi kuwa na wake wengi na kwamba kabla ya kuendeela mbele anapaswa kubadilisha ndoa yake ya kwanza kuwa ya kitamaduni kama inavyofanyika chini ya tamaduni za jamii ya wazulu.

Jaji alitupilia mbali ombi hilo kwa kusema kwamba ,malkia huyo alikuwa nabadili maoni yake baada ya kukubali kwamba mume wake angekuwa na wake zaidi ya mmoja awali.

Alisema kwamba mfalme alikuwa tayari ameshaoa mke wa pili Nozizwe kaMulela ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa benki ya Eswatini mnamo 2022.

Prof Mazibuko ameseka kwamba ndoa yenye wake wengi haikuwa jambo ambalo lilifanyika sana katika jamii ya WaZulu, kwani wafalme wawili wa kwanza hawakuwahi kuoa.

Ila ndoa yenye wake wengi ilikumbatiwa na wafalme waliofuatia Mfalme Misuzulu ndio wa tisa katika jamii ya WaZulu na hali hiyo imekubalika katika jamii hiyo.

'Hivyo ndivyo tunavyojenga familia, hususan familia ya kifalme,' alisema Prof Mazibuko.

Malkia kaMulela anatokea familia yenye umaarufu mkubwa nchini Eswatini, huku ndoa yao ikisemekana ilipangwa kwa ajili ya kuboresha uhusiano mwema kati ya familia mbili za kifalme.

Na japo haipo wazi ikiwa wawili hao bado wana uhusiano, kwa kuwa mfanyakazi huyo wa benki ya Eswatini hajaonekana hadharani katika hafla za kitamaduni za jamii ya Zulu kwa muda sasa wengi wakisema kwamba itifaki kadhaa za kitamaduni katika ndoa yao hazijakamilishwa.

Mfalme wa sasa amekumbwa na matatizo kadhaa ya kindoa , jambo ambalo wengi wanasema limetokana na kanuni za kitamaduni kutofuatiliwa ipasavyo.

Katika ndoa ya mke wa kwanza, mfalme aliamua kufunga ndoa ya kisasa bila ya kufanya ndoa ya kitamaduni.

'Ili ndoa itambulike vuema chini ya tamaduni za Kizulu, ni lazima jamii ikusanyike katika hafla iliyojaa muziki na densi, ' alisema Prof Xulu.

'Wewe kama bibi harusi, ni sharti uwatumbuize waliofika kwa wimbo huku mabinti wanaokusindikiza wacheze nawe, kisha unapaswa kubeba mkuki ambao utampa Mfalme na baada ya hilo, hakuna kurejea nyuma.'

# Cheka tu, simu yako itakuvuruga

**SIMU ya mkononi au rununu ni kifaa kidogo chenye athari kubwa kwa maisha yetu na kwa wanaokitumia vizuri manufaa yake ni makubwa pia .**

Ulimwengu wa teknolojia unamaanisha kwamba matumizi ya simu ya mkononi ni jambo la kawaida na kila mwaka mamilioni ya watu wanaingia katika kundi la wanaoanza kutumia simu za mkononi. Hilo limerahisisha mawasiliano na huduma kote duniani.

Hata hivyo matumizi ya simu za mkononi yanakuja na madhara yake ambayo mwanzoni watu wengi hawakuwa wakijua yanaweza kuvuruga maisha yao sio tu kiafya bali pia kisaikolojia na hata kuhatarisha maisha yao .

Iwapo hukujua kwamba simu hiyo ya mkononi unayotumia kila siku inaweza kuyavuruga maisha yako hizi hapa njia nne ambazo unaweza kujipata pabaya endapo hutakuwa muangalifu au makini kuhusu matumizi yako ya simu .

Kubadili tabia

Kuna ushahidi wa wazi ambao wanasaikolojia wanasema matumizi ya simu yanaweza kuleta mabadiliko kwa tabia ya mtu hasa kijamii.

Sio jambo la ajabu kujua kwamba kwa sasa kuna watu hasa vijana ambao matumizi ya simu yameathiri sana uwezo wao hata kuweza kutangamana kwa njia ya kawaida.

Wamezoea kutumia simu na wakati wasipokuwa na simu zao mkononi maisha kwao yanakuwa sio ya kawaida na hata wanaweza kujihisi wagonjwa. Mara ngapi unazungumza na mtu lakini hata hakuangalii?

Umakini kwenye simu

Hilo hutokana na mazoea ambayo iwapo hayaangaliwi yanaweza kuwa uraibu unaovuruga kabisa jinsi mtu anavyotangamana na wengine kijamii. Je,umewahi kuiweka kando simu yako kwa muda wa saa 24?

Ulihisi ni kama kuna kitu unachokosa maishani mwako? Basi kuna watu wasioweza kuendelea na shughuli zao kamwe bila kuwa na simu zao mikononi.

Visa pia ni vingi vya watoto majumbani kuachwa hoi wakati wazazi wanapojishughulisha na simu zao za mikononi na kukosa kuwapa hata muda wa kuwasikiza au kucheza nao.

**Kujisahaulisha**

Umeskia kuhusu ajali za barabarani zinazosababishwa na madereva ambao wanaendesha gari wakitumia simu za mkononi. Takwimu ni nyingi kuhusu idadi ya maafa yanayosababishwa na ajali kama hizo.

Kumekuwa na kampeni kote duniani na hasa kutoka kwa polisi kuhusu hatari ya kuendesha gari ukitumia simu.

Visa pia vipo kuhusu watu ambao wanafanya kazi zinazoweza kutajwa kama 'hatari' ambao wanajitia hatarini hata zaidi kwa kutumia simu.

Iwapo utajipata katika hali kama hizo,unashauriwa kuiweka kando simu yako mpaka ufike hatua unayoweza kuitumia. Ujumbe huo, simu hiyo au hata video hiyo unaweza kuishughulikia baada ya safari yako au ukiwa salama.

Basi ikiwa ulifikiri simu ya mkononi haiwezi kukutia hatarini kwa njia hii basi ujumbe huu utakupa fursa ya kutafakari matumizi ya simu yako

Fedha siyo zako?

Umeyasikia hayo kuhusu watu kuzitumia simu vibaya kwa kutoa fedha wanazotumiwa kimakosa.

Kwa muda mrefu watu wamekuwa wakitumia simu kama kinga ya kufanya maovu na uhalifu. Sheria zinabadilika na kuboreshwa na usije ukadanganyika kwamba unaweza kutekeleza uhalifu kutumia simu yako ukifikiri uko salama.

Nchini Kenya kwa mfano mwanamke mmoja yupo mashakani kwani huenda akafungwa jela kwa kutoa Sh 271,200 alizotumiwa kimakosa katika akaunti yake ya mpesa kupitia simu.

Elizabeth Karimi inaripotiwa na vyombo vya habari nchini humo alitumiwa fedha hizo kwa bahati mbaya na mtu aliyekosea nambari ya akaunti. Wakati kampuni husika zilipojaribu kuzirejesha fedha hizo, Kirimi alikuwa ameshazitoa fedha hizo kutoka kwa akaunti yake. Baadaye kesi hiyo ilifikishwa polisi na akasakwa, kukamatwa na kufikishwa kortini.






# Mafia inatubeba kwa mengi



**JE unamjua Papa Potwe? (Whale Shark) ni Samaki mkubwa duniani na huweza kufikia hadi mita 18. Akiwa mdogo huwa na kimo cha basi dogo la abiria.**

Samaki hawa hupatikana maeneo machache duniani, na kwa mujibu wa watafiti wa bahari ni miongoni mwa viumbe vilivyopo hatarini kutoweka.

Moja ya maeneo wanayopatikana ni kisiwani Mafia Tanzania, sehemu nyingine ni kama Mexico na Philipenes.

Katika maeneo ya ufukwe wa Mafia mjini, naambiwa kuwa samaki hawa wakubwa duniani ikifika msimu wake basi huonekana hata ukiwa ufukweni, huna haja ya kuingia baharini labda tu ukitaka kuogelea nao.

Papa Potwe hujulikana pia kama Papa mwema kwa ukarimu wake, hufuata wavuvi na watalii wakiwa ndani ya maji na hucheza nao.

Kwa kipindi cha mwaka mmoja Papa Potwe huweza kusafiri hadi kilomita 10,000. Lakini watafiti wanasema kuwa Papa Potwe wa kisiwani mafia hubaki eneo moja kwa muda mrefu. Katika makala ya National Geographic mtafiti kutoka Marekani, Simon Pierce anasema kuwa hawaendi mbali na inakua kama wanawatembelea rafiki zao wa zamani.

"Hakuna sehemu nyingi ambapo unaweza kuwaona Papa Potwe wale wale kila mara, na inakua kama utamtembelea rafiki yako wa zamani" anasema Simon

Kwa upande wa wavuvi wao wenyewe wametengeneza vikundi vya ulinzi shirikishi na jukumu la kwanza ni kuwalinda samaki hawa adimu, kutokana na asili ya samaki hawa hutembea na makundi ya samaki wengi wadogo hivyo ni fursa kwa wavuvi.

Wavuvi niliozungumza nao wanasema kuwa samaki huyu, kwao hana msimu wanamuona kila siku .

Said Isaa Kombo ni mwenyekiti wa ulinzi shirikishi kwa rasilimali za bahari na ni mvuvi, anasema kuwa mara nyingi hukutana na samaki huyu wakati mwingine wanalazimika kuachia samaki waliwavua ili tuu wampishe wala wasimdhuru samaki huyu.

"kama akivuta nyavu zetu na asiweze kujitoa basi tunalazimika kuwasamehe wale samaki wote tuliowavua na kumuacha aende"

Mbali na jitihada zinazofanyika lakini bado Samaki hawa wanakumbwa na hatari kubwa kutokana na shughuli za uvuvi., na kama jitihada za ziada zisipofanyika basi itabaki historia kuwa kulikuwa na Samaki wakubwa duniani.

# Hizi ndizo faida za wanyama pori

**WANYAMA pori ni viumbe wanaoishi katika mazingira yao asilia bila kufungwa na binadamu.**

Hawa ni pamoja na aina nyingi za mamalia, ndege, reptilia, na wadudu ambao wanapatikana katika misitu, savanna, milima, mabonde na hata katika maeneo ya maji kama mito na bahari.

Wanyama pori wana mchango mkubwa sana kwa mazingira, uchumi, na jamii kwa ujumla. Kutambua faida na umuhimu wa wanyama pori ni muhimu katika juhudi za kutunza na kulinda maliasili hizi muhimu.

**1. Faida**

Wanyama pori husaidia kuimarisha mfumo wa ikolojia kwa kudhibiti idadi ya viumbe mbalimbali katika mnyororo wa chakula. Kwa mfano, wanyama walaji-nyasi (herbivores) kama nyati na pundamilia hula nyasi na kupunguza msongamano wa mimea, hivyo kusaidia katika kudhibiti ukuaji wa mimea.

Wanyama wanaokula nyama (carnivores) kama simba na chui husaidia kudhibiti idadi ya wanyama wanaokula nyasi, na hii inasaidia kuhifadhi uwiano katika mazingira.

Wanyama pori kama tembo, ndege, na wadudu husaidia katika usambazaji wa mbegu za mimea wanapohama kutoka eneo moja kwenda jingine.

Hii ni muhimu kwa kuendeleza msitu na kuimarisha uoto wa asili katika maeneo mbalimbali ambayo nayo husaidia kuhifadhi rutuba ya ardhi na hewa safi.

Baadhi ya wanyama pori kama vile wadudu wa ardhini huchangia katika kuongeza rutuba ya udongo kwa kuchimbua na kuchanganya udongo.

Hii inasaidia mimea kukua kwa urahisi na kudumisha uzalishaji wa chakula katika ikolojia ya asili. Msitu na maeneo yenye mimea mingi ambayo yanatunzwa na wanyama pori yanaweza kufyonza dioksidi kaboni ($CO_2$) kutoka angani.

Wanyama pori, hasa wale wanaosaidia ukuaji wa msitu, husaidia katika kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kuhifadhi hewa safi na kupunguza uzalishaji wa gesi zinazochafua mazingira.

**2. Umuhimu**

Nchi nyingi, hasa katika Afrika, hutegemea utalii wa wanyama pori kama chanzo kikuu cha mapato. Watalii kutoka nchi mbalimbali huja kushuhudia uzuri wa wanyama pori kama vile tembo, twiga, simba, na faru.

Hii inachangia mapato kupitia ada za kuingilia hifadhi, malazi, na usafiri. Mapato haya yanasaidia serikali na jamii katika kujenga miundombinu na huduma za kijamii.

Utalii wa wanyama pori huunda nafasi nyingi za ajira kwa wenyeji kama vile waongozaji wa watalii, walinzi wa wanyama, wapishi na wafanyakazi wa hoteli. Hii inasaidia kuboresha maisha ya jamii zinazozunguka hifadhi za wanyama pori na kusaidia kuboresha uchumi wa eneo husika.

Jamii zingine hutegemea wanyama pori kama chanzo cha vyakula vya asili, ingawa hili linapaswa kufanywa kwa kuzingatia sheria na kanuni za uhifadhi.

Wanyama pori kama samaki na ndege huchangia katika upatikanaji wa protini kwa jamii husika, ingawa ni muhimu kuhakikisha kuwa unawindwa kwa njia endelevu ili wasitoweke.

Baadhi ya jamii zinatumia wanyama pori kama chanzo cha dawa za asili kwa ajili ya tiba za kitamaduni. Hii inajumuisha matumizi ya mafuta, ngozi, na mifupa ya wanyama pori katika tiba asilia, ingawa ni muhimu kuzingatia sheria za uhifadhi na kuzitumia kwa kiasi kidogo ili kuzuia kutoweka kwa aina za wanyama.

**3. Umuhimu**

Wanyama pori wanashikilia nafasi muhimu katika tamaduni nyingi. Wanyama kama simba, tembo, na chui wanaonekana kama alama za nguvu na ushupavu, na mara nyingi huchukuliwa kama sehemu ya urithi wa kitamaduni wa jamii.

Jamii nyingi zinaaminika kurithi hekima na ujasiri kutoka kwa wanyama hawa.

Kuwatazama wanyama pori katika makazi yao ya asili ni burudani na husaidia watu kujifunza zaidi kuhusu mazingira. Hii hujenga uelewa wa umuhimu wa wanyama pori na hitaji la kuwahifadhi.

Watoto na vijana wanaweza kufundishwa kuhusu uhifadhi na jinsi wanyama pori wanavyohusiana na maisha ya binadamu, jambo ambalo linaweza kuwafanya kuwa wahifadhi wazuri wa maliasili hapo baadaye.

Kutembelea hifadhi za wanyama pori kunaweza kusaidia kupunguza msongo wa mawazo na kuboresha afya ya akili. Mazingira ya asili yanapotembelezwa kwa utulivu na kuzungukwa na wanyama pori, watu hupata fursa ya kupumzika na kujisikia karibu na asili.

Hii husaidia kuboresha afya ya akili na kupunguza msongo wa mawazo.

**4. Changamoto**

Ujangili ni mojawapo ya changamoto kubwa inayowakabili wanyama pori, ambapo baadhi ya watu huwaua kwa ajili ya kupata pembe, ngozi, na sehemu nyingine za mwili ambazo zinauzwa kwa bei kubwa kwenye soko la kimataifa.





# Huyu ndiye Mbega usiyemjua

**NENO Mbega ( Colubus) limetokana na neno la Kigiriki likiwa na maana mnyama jamii ya nyani mwenye vidole vinne pasipokuwa na kidole gumba.**

Mbega weupe na weusi ni viumbe jamii ya nyani wanaopatikana barani Afrika ambapo kuna aina kuu mbili ambazo kwa majina ya kitaalamu hujulikana kama (Colubus angolensins) na (Colubus gueleza) aina hizi mbili zinapatikana Tanzania.

Lakini pia kuna makundi madogo madogo ya wanyama hawa wakuvutia , Mbega ni wazawa na wanapatikana Bara la Afrika pekee, hususani ukanda wa nchi za Afrika mashariki na kati.

Mbega aina ya (Colubus angolensis) hawana tofauti kubwa na (Colobus guereza). Mbega hawa wana rangi nyeupe na nyeusi, ambapo rangi nyeupe huonekana maeneo ya mabegani na maeneo ya usoni ndio maana tunawaita mbega weupe na weusi.

Mbega aina ya (Colobus guereza), ameunda umbo linalo fanana na herufi U ingawa sio kamili ukimuangalia kwa makini utagundua hilo, rangi hiyo nyeupe inaanzia bega moja kwenda mkiani hadi bega lingine ingawa sehemu za mkiani haija kolea sana na sehemu kubwa ya uso kwenye mashavu, na masikioni. Lakini mbega wa aina ya (Colubus angolensis) wana alama nyeupe ambazo zina bembea mabegani na sehemu chache za usoni weupe huo haupo masikioni hiyo ndio tofauti yake kubwa.

Kuna mbega weupe na weusi wanaopatikana ukanda wa Afrika mashariki ( Colubus guereza) ambao mengi nitakayo zungumia yatamgusa pia (Colubus angolensis) kwa uchache kwa sababu tabia zao na maisha yao kwa ujumla hufanana kwa asilimia kubwa, tofauti kubwa ni hiyo ya muonekano wa nje.

Mnyama huyu anapatikana maeneo mengi Tanzania, hasa yaliyohifadhiwa kama hifadhi za Taifa, mapori ya akiba, hifadhi za jamii, na hata maeneo yasiyo hifadhiwa nchini Tanzania

**SIFA, TABIA ZA MBEGA**

Kama nilivyotangulia kusema kwenye utangulizi mbega utamjua kwanza kwa kuona rangi za kuvutia nyeupe na nyeusi. Ambapo rangi nyeusi inachukua sehemu kubwa ya mwili wa mbega, rangi nyeupe kuongeza mngao ambao ndio hubeba maana halisi ya jina la Mbega weupe na weusi.

Mabegani, mashavu, shingo, paji la uso na kwenye ncha za mikia wana rangi nyeupe. Mbega wana vidole vinne, hawana kidole gumba tofauti na jamii nyingine ya nyani.

Mbega dume ana umbo kubwa kidogo ukilinganisha na mbega jike. Wana mikia mirefu yenye rangi nyeusi, ambapo mwisho una rangi nyeupe.

Ana macho meusi na makubwa yanayoona vizuri, pia wana masikio makubwa kuwawezesha kusikia vizuri. Mbega hawana tabia ya wizi kama aina nyingine ya nyani kwa sababu ya tabia yao ya uchaguzi wa chakula.

Mbega hutumia muda wa nusu siku wakiwa wamejipumzisha, na muda uliobaki huutumia kutafuta chakula na kucheza juu ya miti kwa madaha. Hivyo unaweza kuwaona muda wa asubuhi sana na jioni jua likiwa limetua.

Wanaishi katika makundi madogo ambayo yanakua na mwanaume mmoja ambaye ndio baba wa familia na wanawake kuanzia watatu hadi wanne pamoja na kundi rika lenye vijana na mbega

Muda wa usiku wanalala pamoja kama ilivyo kawaida ya familia, huku wakijitawanya kwenye miti ambayo hujipatia chakula kwa urahisi zaidi

Kila kundi lina mipaka ya kifamilia inayoeleweka, huwasiliana kwa kutumia ishara na sauti mbalimbali kama kuna uvamizi umetokea, kuweka nafasi kati ya kundi moja na jingine, kuimarisha ulinzi katika kundi pia kuonyesha utawala wa kundi husika.

Mbega hupendelea sana kukaa juu ya miti, ni nadra sana kuwaona ardhini, kwenye miti wanauwezo wa kuruka toka mti mmoja hadi mwingine kwa madaha umbali upatao Mita 15 ambazo ni sawa na futi 50 bila hofu yoyote, ina aminika manyoya yanayo ninginia mabegani na mkia ndio huwa kama mwamvuli (parachuti) kuzuia wasiweze kuanguka kwa umbali mrefu wanaoweza kuruka.

Mbega wana uzito upatao kilogram 4 hadi 14 na urefu upatao sentimita 75,

**WASTANI WA MAISHA**

Kwa wastani maisha ya mbega weupe na weusi ni miaka 20 wakiwa porini na miaka 25 hadi 30 wakiwa kwenye uangalizi maalumu 'Captivity', wakiwa msituni au mazingira yake ya asili, wanakabiliana na changamoto mbalimbali kama kujilinda dhidi ya maadui, uwezo wa kukabiliana na magonjwa, na changamoto za utafutaji wa chakula na pia hutegemea sana majani machanga ya miti na baadhi ya matunda machanga hivyo hufupisha wastani wa maisha yake.

Mbega wana makundi maalumu na mipaka inayofahamika kutofautisha kati ya kundi moja la mbega na kundi jingine, ukubwa wa eneo yapata hekari 40 kwa kila kundi, ambapo linatengenezwa na dume la mbega mmoja, wanawake kuanzia wa 3 hadi 4, vijana, pamoja na watoto.

Hivyo idadi yao hukamilika kukiwa na kundi lenye wastani wa mbega wa 5 hadi 10 katika kundi moja, dume la mbega hao likiwa ndio kiongozi wa familia kwa kuweka mipaka na kuhakikisha ulinzi wa kundi hilo.

# 'Suti ya Zelensky' yazua mjadala

**IJUMAA ya Februari 28, mwaka huu haikuwa siku rahisi kwa Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky alipotembelea Ikulu ya White House, Washington DC, Marekani.**

Kabla hata ya mzozo ulioibuka kati yake na wenyeji wake Rais Donald Trump na Makamu wa Rais JD Vance mbele ya waandishi wa habari, Trump alimpokea Zelensky mlangoni na kuwaambia waandishi wa habari 'leo amevalia kweli kweli'.

Baadhi walitafsiri hii si kama sifa bali kijembe kwa Zelensky ambaye alikuwa amevaa fulana nyeusi ya mikono mirefu.

Wakati Trump anampokea Waziri Mkuu wa Uingereza Keir Starmer, alionekana akiyaangalia mavazi ya kiongozi huyo kuanzia juu hadi chini, huku akinong'ona maneno yanayoweza kutafsiriwa kama sifa kwa suti aliyokuwa ameivaa Starmer.

Baada ya malumbano kati ya Zelensky, Trump, Vance na waandishi wa habari kukaribishwa kuuliza maswali, mwandishi Brian Glenn kutoka Real America's Voice chombo kinachoegemea mlengo wa kulia aliuliza kuhusu mavazi ya Zelensky

"Kwanini hauvai suti? Upo katika ofisi ya juu kabisa katika nchi hii, na umegoma kuvaa suti, huna suti?" Aliuliza Glenn.

Kwa upole, Zelensky alimjibu atavaa suti pale vita vitakapomalizika.

"Nitavaa suti vita hivi vitakapomalizika. Labda suti kama yako, labda bora zaidi ya hiyo yako, au labda ya bei nafuu kuliko yako," alisema Zelensky.

Swali hilo la Glenn limeibua mjadala mkubwa mitandaoni huku baadhi wakimuunga mkono mwandishi aliyeuliza huku wengine wakimkosoa kwamba amefanya dhihaka.

Mbunge wa Jimbo la Georgia ambaye pia ni mchumba wa mwandishi huyo aliandika katika mtandao wa X kwamba amejisikia fahari kwamba Glenn ameuliza swali hilo.

"Ninajivunia sana @brianglenntv kuonyesha kwamba Zelensky hana heshima kwa Marekani kiasi kwamba hawezi hata kuvaa suti katika Ofisi ya Oval anapokuja kuomba pesa kutoka kwa Rais wetu!!" aliandika Marjorie Taylor Greene.

Hata hivyo mwandishi wa habari machachari kutoka Uingereza na rafiki wa karibu wa Donald Trump, Piers Morgan alilikosoa swali hilo na kusema Zelensky si pekee aliyekwenda ofisi ya rais bila kubaa suti. "Swali la kipuuzi. Elon Musk havai suti anapoingia ikulu?" Aliandika Morgan.

Wanahistoria wanakumbusha pia kwamba Waziri Mkuu wa zamani wa Uingereza Winston Churchil aliwahi kufika ofisi ya Rais wa Marekani ijulikanayo kama 'Oval Office' katika ziara rasmi bila ya kuwa amevaa suti.

Tangu kuanza kwa vita nchini Ukraine, Zelensky ameepuka kuvaa suti karibu katika ziara zake za nje ya nchi na hata pale anapokuwa ametembelea na viongozi mbalimbali kutoka nje ya nchi yake.

Tangu nchi yake kuvamiwa na Urusi mwaka 2022, Zelensky amekuwa akipendelea kuvaa aidha tisheti na suruali ya kijeshi zote zikiwa za kijani kibichi au vya rangi nyeusi kama aliyokwenda nayo Ikulu ya Marekani.

Zipo tafsiri kadhaa zilizotolewa juu ya aina ya vazi analopendelea kuvaa hivi sasa Zelensky ikiwa ni pamoja na kutoa ishara ya hali tete na ya dharura inayoendelea nchini mwake

Sababu nyingine inasemwa ni ujumbe wa mshikamano ambao Zelensky anauonyesha kwa wanajeshi wa nchi yake walio mstari wa mbele wa mapambano.

Lakini pia Zelensky anataka kutuma ujumbe kwamba yeye si kiongozi anayevaa suti, na kuongoza nchi yake kwa mbali, bali ni kiongozi anayeshiriki moja kwa moja katika mapambano ya kuilinda nchi yake

Hata kabla ya uvamizi wa Urusi nchini mwake, akiwa kiongozi aliyetokea katika fani ya ucheshi na si mwanasiasa wa kawaida, Zelensky anaelezwa kupendelea kwenda tofauti na mazoea ya siasa si tu katika mavazi yake lakini hata katika namna anavyoiongoza.





# NICK POPE KUUZWA



LONDON, England

**NEWCASTLE ikotayari kumuuza mlinda lango wao wa Uingereza Nick Pope, 32, kwa kati ya pauni milioni 10-15 na wana nia ya kumbadilisha na kipa wa Burnley mwenye umri wa miaka 22 James Trafford.**

Barcelona inatazamia kuongeza mkataba wa winga wa Brazil Raphinha, 28.

Nayo Chelsea bado iko mbioni kumsaka kiungo wa Gremio na Brazil Gabriel Mec, 16.

## BARCA KWA GARNACHO

OSIMHEN RADA MAN UNITED

MANCHESTER, England

**TIMU ya Manchester United inataka kumsajili mshambuliaji wa Nigeria Victor Osimhen, 26, kutoka Napoli, ambayo inatathmini uwezekano wa kumpata mshambuliaji wa Denmark Rasmus Hojlund, 22, kama sehemu ya mkataba huo.**

Wakati huo huo, Manchester United ina mpango wa kumnunua kiungo wa Real Sociedad na Uhispania Martin Zubimendi, 26.

## TRINCAO VITA TUPU



**MANCHESTER, England**

**MANCHESTER City na Manchester United zinamfuatilia kwa karibu winga wa Ureno Francisco Trincao, ingawa Sporting ina matumaini ya kufikia kandarasi mpya na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25.**

**Nayo Everton inataka kumsajili winga wa Brazil Luis Henrique, 23, kutoka Marseille msimu huu wa joto lakini watakabiliana na ushindani kutoka kwa Newcastle na Nottingham Forest**

## WINTER ATAKIWA WEST HAM

LONDON, England

**WEST Ham wana nia ya kumsajili beki wa Genoa wa Mbelgiji Koni de Winter, 22.**

Nazo Tottenham na Brighton ni miongoni mwa vilabu kadhaa vinavyowania saini ya beki wa Romania Andrei Ratiu, 26, anayekipiga katika klabu ya Rayo Vallecano.

## GAEI JICHO LA LIVERPOOL

LIVERPOOL, England

LIVERPOOL inamfuatilia beki wa Denmark Anton Gaaei, 22, na mshambuliaji wa Ubelgiji Mika Godts, 19.

Tottenham iko tayari kuongeza dau lao ka pauni milioni 8.5 kumsajili mshambuliaji wa Ujerumani Timo Werner msimu huu wa joto baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kuondoka RB Leipzig kwa mkopo.

BUSATI
MICHEZO
JUMANNE MACHI 4, 2025
Tovuti: www.tanzaniabora.co.tz




# WAKALI WAO!

## >> WAKIONA NYAVU TU LAZIMA UMWAGE CHOZI

NA MWANDISHI WETU

**NDANI ya Ligi Kuu Bara ambayo ni namba nne kwa ubora Afrika kuna wakali wakucheka na nyavu ambao wameandika rekodi zao za kusepa na mipira Bongo msimu wa 2024/25.**

Nyota wa kwanza kufunga hat trick ndani ya ligi ni Prince Dube ambaye yupo ndani ya kikosi cha Yanga huyu alifunga kwenye mchezo dhidi ya Mashujaa, Uwanja wa KMC Complex waliposhuhudia ubao ukisoma Yanga 3-2 Mashujaa.

Yanga ni namba moja kwenye eneo la kucheka na nyavu Bongo ambapo safu ya ushambuliaji imetupia mabao 58 na pointi zao kibindoni ni 58 ikiwa inaongoza ligi.

Mkali wa pili kucheka na nyavu akiwa na hat trick ni Aziz Ki ambaye huyu alifunga kwenye mchezo dhidi ya KMC walipoibuka na ushindi wa mabao 6-1 Uwanja wa KMC Complex.

Yanga hat trick zote zimekusanywa Uwanja wa KMC Complex ambapo mchezo mmoja dhidi ya Mashujaa walikuwa nyumbani na mchezo mwingine dhidi ya KMC walikuwa ugenini.

Nyota mwingine ni Steven Mukwala huyu wa Simba alifunga mbele ya Coastal Union, Machi Mosi 2025 Uwanja wa Sheikh Amri Abeid ubao uliposoma Coastal Union 0-3 Simba.

Kituo kinachofuata ni Machi 8, Yanga v Simba, Uwanja wa Mkapa wakali hawa wanatarajiwa kukutana msako wa pointi tatu.

## MUKWALA ANAWASALIMIA HUKO

NA MWANDISHI WETU

**MWAMBA Steven Mukwala ameandika rekodi yake ya kuwa nyota wa kwanza kufunga hat trick ndani ya kikosi cha Simba kwa msimu wa 2024/25 ukiwa ni msimu wake wa kwanza.**

Nyota huyo anayevaa jezi namba 11 alifanya hivyo kwenye mchezo wa ligi dhidi ya Coastal Union uliochezwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid ilikuwa Machi Mosi 2025 baada ya dakika 90 ubao ukasoma Coastal Union 0-3 Simba.

Simba mbele ya Coastal Union msimu wa 2024/25 imekomba pointi nne mchezo wa mzunguko wa kwanza walitoshana nguvu kwa ubao wa Uwanja wa KMC, kusoma Simba 2-2 Coastal Union.

Baada ya kufunga mabao matatu anafikisha mabao 8 katika Ligi Kuu Bara ambayo ni namba nne kwa ubora Afrika huku Simba ikiwa nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi na pointi 54 vinara ni Yanga wenye pointi 58.

Leonel Ateba naye ana mabao 8 kinara ndani ya kikosi cha Simba kwenye kucheka na nyavu ni Jean Ahoua mwenye mabao 10 kama namba ya jezi yake ila huyu ni kiungo mshambuliaji.

Kazi bado inaendelea kwenye ligi ambapo kituo kinachofuata kwenye mchezo ujao wa ligi ni dhidi ya Yanga unaotarajiwa kuchezwa Machi 8 2025, Uwanja wa Mkapa, Dar es Salaam.